# LEARNING BY EAR

## Lent Luxury-The risks of raising credit

## EPISODE TEN: THE CONCLUSION

**AUTHOR: James Muhando**

**EDITORS: Adrian Kriesch, Friederike Müller**

**PROOFREADER: Tony Dunham**

**Kisuaheli: Eric Ponda**

**<u>LIST OF CHARACTERS BY SCENE.</u>**

**<u>SCENE ONE: AT UNCLE BARRY'S GROCERY.</u>**

- **CUSTOMER (M/F AGE NOT IMPORTANT).**
- **UNCLE BARRY (OLDER THAN 45 NOW).**
- **GIDDY (M NOW 30) = Narrator**
- **BUYER (F 30'S).**
- **3-5 JUICE DRINKERS (AGE NOT IMPORTANT).**

**SCENE TWO: DAYTIME, AT KWANZA PUB.**

- **3-5 DRUNKS (MALE ADULTS).**
- **BENSON (M ADULT).**
- **MAMA PIMA (F 40'S).**
- **JD (MALE NOW 30).**

**SCENE THREE: AT UNCLE BARRY'S GROCERY.**

- **UNCLE BARRY (OLDER THAN 45).**
- **GIDDY(NOW 30) = Narrator**
- **JD (NOW 30).**
- **3 JUICE DRINKERS.**

**SCENE FOUR: AT THE BAR**

- **JD (M NOW 30)**
- **GIDDY (NOW 30) = Narrator**
- **MAMA PIMA(F 40'S)**
- **3-5 DRUNKS**

INTRO:

---

**1. SFX: VILLAGE AMBIENCE, FOOTSTEPS**

**2. NARRATOR:**

Hujambo na kwa mara nyingine tena karibu katika mfululizo wa vipindi vya " Learning By Ear" '**Noa Bongo Jenga Maisha yako'**. Hii ni sehemu ya kumi na ya mwisho kwenye mchezo huu wa Redio kuhusu "**Starehe za Kuazima- Tatizo la Kulipa Mkopo**". Jina langu ni Gideon Leboo, ofisa wa masuala ya Mikopo katika Benki hii ya Jubillee, na pia mhusika mkuu katika mchezo huu. Ningependa kukurejesha nyuma kidogo kuzungumzia kijiji nilichozaliwa. Tangu mchezo huu wa redio uanze, nimekuwa nikikutana na wewe ofisini kwangu na kukuelezea kuhusu maisha ya ujana wangu. (**Happy**) Lakini baada ya kuishi nje ya kijiji hicho kwa muda wa miaka mingi sasa, nimeamua kurudi nyumbani. Nafurahi sana kurudi nyumbani ili kuvuta tena hewa nzuri, mazingira na kila kitu. Kwa hakika napenda sana mazingira ya kijiji chetu ... Ahh ...hebu tazama yule pale..! Ni mjomba Barry akiuza bidhaa katika kibanda chake. Hebu twende tukamtembelee, labda pengine tayari amekuwa fukara..(laughs)…

## SCENE ONE: UNCLE BARRY'S GROCERY

**3.** **SFX:** **DOOR OPENS**

**4.** **SFX:** **SHOP/CAFE ATMO (BARRY'S GROCERY), CUSTOMERS DRINKING JUICE**

**5.** **CUSTOMER1:** Mjomba Barry juisi yako ni tamu, na tena *freshi* kabisa! Unaweza kuniongezea tafadhali?

**6.** **BARRY:** Bila shaka!

**7.** **GIDDY:** Habari ya asubuhi Bw. Leboo.

**8.** **BARRY:** Nzuri ...! Karibu hapa tunapouza kila aina ya matunda, maembe, machungwa na kadhalika....

**(Realises it is Giddy)** Giddy, njoo hapa! Usinichezee jinsi hiyo! Unataka kunipa maradhi ya moyo? Naona umebadilika sana!

**9.** **THEY LAUGH**

***KW begin***

**10.** **GIDDY:** **(Jokes)** Kwa nini maradhi ya moyo mjomba Barry? Kwani bado unadaiwa, na unataka kuwatoroka wadeni wako?

11. **BARRY:** **(Laughs)** Njoo hapa nikukumbatie! Habari za siku nyingi mtoto wangu?

12. **SFX: RUSTLE OF CLOTHES AS THEY HUG.**

13. **GIDDY:** Mimi ni mzima kama ...

14. **BUYER:** **(Interrupts)** Mjomba Barry! Kilo mbili za ndizi, mbili za machungwa na mbili za maembe tafadhali!

15. **BARRY:** Habari mama Lulu! Kilo mbili za ndizi, mbili za machungwa na mbili za Maembe..? sawa utapata sasa hivi!. Ni dola 4.

16. **SFX:** **PAPER BAG AND MONEY EXCHANGE HANDS.**

***KW end***

17. **BARRY:** **(To Giddy)** Subiri ...Keti hapo kwa kiti dakika chache tu mtoto wangu! Utakunywa nini, juisi ya maembe au, machungwa..?

18. **GIDDY:** Wewe mwenyewe unajua napenda sana juisi ya maembe, mjomba!

19. **BARRY:** Ni kitambo,.. nimeanza kusahau! Nadhani nikuzeeka sasa!

20. **THEY LAUGH**

21. **SFX:** **JUICER TURNED ON THEN OFF**

**22. SFX: GLASS PUT ON TABLE**

**23. BARRY:** Hii hapa!.

**24. GIDDY:** Asante sana! Naona biashara yako inaendelea vizuri sana**.** Inatia moyo kuona jinsi ulivyobadilika, sio tu kibiashara bali tabia na maisha kwa jumla!

**25. BARRY:** Najaribu kupambana na maisha mwangu!

**26. GIDDY:** Lakini ni vipi ulivyoweza kujinasua kutoka ile tabia iliyokuwa imekutawala ya kuombaomba au kuchukua mikopo hovyo hovyo? Nakumbuka ulivyokuwa ukiishi maisha ya kukata tamaa!

***KW begin***

**27. BARRY:** **(Chuckles)** Sio tu maisha ya kukata tamaa! Wala nisingeweza kujisaidia kabisa**!** Lakini yote ni kujitolea. Jambo ambalo sitasahau, mamako na mafariki zangu waliendelea kunisaidia hata nikiwa gerezani, baada ya kufungwa kwa kukosa kulipa madeni, utapeli na kuwaibia watu. Ni jambo la kusikitisha sana.

**28. GIDDY:** **(Laughs)** Nakumbuka enzi hizo! Lakini, ni vipi uliweza kujitoa katika maisha haya?

***KW end***

29. **BARRY:** Nilipata ushauri wa kitalaam nilipokuwa gerezani. Ushauri kutoka kwa waatalam wa masula ya kifedha uliotufunza jinsi Mtu anavyoweza kuishi kadri ya uwezo wake.

30. **GIDDY:** Na ushauri huo ulikusaidia vipi kuepukana na tabia hii ya kujilimbikizia madeni?

31. **BARRY:** Kuishi kadri ya uwezo wako hakumaanishi kwamba ni lazima uishi kwa madeni. Lakini unaweza kukopa. Hata mimi bado nakopa. Lakini nakopa kwa lengo la kuimarisha biashara yangu!

32. **CUSTOMER1:** **(Off mic)** Mjomba Barry, pesa zako hizi!

33. **BARRY:** Subiri nitarudi sasa hivi!

34. **SFX:** **FOOTSTEPS LEAVE**

35. **GIDDY:** Hakuna neno, biashara kwanza! **(addresses listeners)** Mjomba Barry… ! Nani aliyefikiri kwamba siku moja atakuja kubadilika na kushika mkondo mzuri wa maisha? Watu hubadilika, mfano miaka michache iliyopita, nilikutana na rafiki yangu Jenny. Siku hizi anasimamia biashara yake ya uchukuzi, ..! ehhe.. Biashara ya uchukuzi wa malori, pick-ups.. na kadhalika...! Ama kwa hakika amefaulu maishani! Lakini, pia akanieleza kuhusu

mtu mwengine ambaye hajabadilika kabisa. Kwa maneno ya kuambiwa, mtu huyo ni mlevi kupindukia mjini humo…

**SCENE TWO: AT KWANZA PUB**

**36. SFX: Backflash-sound**

**37. ATMO: BAR ATMO, DRUNK NOISES**

***KW begin***

**38. BENSON:** Mama Pima, leo wewe ni goigoi sana! Kwani hutaki pesa zangu?

**39. MAMA PIMA:** Benson. Kwani umemuibia tena mkeo leo kuja kunywa pombe?

**40. DRUNKS: (LAUGH)**

**41. BENSON: (Tipsy)** Lakini bora si nakulipa! Tatizo lako ni kulipwa au kujua nilikozitoa hizi pesa!

**42. DRUNKS: LAUGH.**

**43. SFX: FOOTSTEPS APPROACH.**

***KW end***

**44. JD: (Drunk, roars like a lion)** Weee,...! Simba amewasili! Mama Pima nipe chupa moja ya pombe!

45. **MAMA PIMA:** Hebu mtazame huyu! Asubuhi na mapema na tayari amelewa chakari. Kwanza nilipe zile chupa zangu saba ulizokunywa JD!

46. **JD:** Wewe mwanamke ! Unamuita nani mlevi? Niletee pombe hapa!…

47. **MAMA PIMA: (Firm)** Kama sitakupa utanifanya nini? Toka nje upesi!

48. **JD:** Siondoki! Siendi kokote!

49. **MAMA PIMA: (Sarcasm)** Una uhakika! Sawa tutaona!

50. **SFX: FOOTSTEPS.**

51. **JD:** Usinikaribie! Mimi nimepata mkanda mweusi wa kupigana karate.Usijaribu.. ni....

52. **MAMA PIMA:** Mkanda mweusi!

53. **SFX: PUNCHES HIM. HE FALLS OUT OF THE BAR.**

54. **DRUNKS: LAUGH & COMMENT.**

55. **JD: (Complains from outside)**

56. **MAMA PIMA:** Kaa huko nje! Bure kabisa wewe! Mwanaume gani wewe..! Siku hizi wanawake wanazaa wanaume wa aina gani? Huyu kijana hata hajafikisha umri wa miaka 30 na amezeeka kama mtu wa miaka 70! Kazi yake ni kunywa pombe hapa bila kulipa!

**57. SFX: Backflash-sound**

**SCENE THREE: UNCLE BARRY'S GROCERY.**

**58. ATMO: SHOP/CAFE ATMO (BARRY'S GROCERY), CUSTOMERS DRINK JUICE**

**59. GIDDY:** **(to himself)** Maskini JD!, Haya ndio maisha ya mjini niliyokuwa nikiambiwa! Kuingia na kutoka baa moja hadi nyingine, kuywa pombe bila kulipa! Pesa zote zinaishia kunywa pombe tu!

**60. SFX: FOOTSTEPS APPROACH**

**61. U. BARRY: (as he approaches)** Wewe,.! Kwanini unaongea peke yako! Tuko wapi? Ah ndio..! Sasa kwanini umeniuliza maswali hayo yote jinsi nilivyoepukana na madeni na mikopo, Gideon?

**62. GIDDY:** Nilitaka kusikia kutoka kwako. Na kwa sababu ya kazi ninayofanya, ni vyema kufahamu maisha ya mtu anayezungukwa na madeni. **(PAUSE)** Niambie, baada ya kupitia maisha hayo, kufungiwa nyumba ,kupigwa na

wakora na hatimaye kufungwa gerezani, unaweza kumshauri mtu achukue mkopo?

**63. U. BARRY: It's better** Akiweza bora mtu ajiepushe na mikopo! Lakini sioni tatizo la kuchukua mkopo mimi! Wewe kama afisa wa masuala ya mikopo, unafahamu vyema hilo! Makosa watu wanayofanya mimi nikiwa mmoja wao ni kukosa mwelekeo. Au kuchukua mkopo kwa sababu pesa ziko.

***KW begin***

**64. GIDDY:** Kumaanisha ?

**65. BARRY:** Utafiti unaonyesha kuwa watu wengi wanashindwa kulipa mikopo, kwa sababu kwanza huwa hawana mipango maalum na pesa hizo. Au baada ya kupata pesa hizo huishia kuzitumia kwa malengo ambayo hawakuyakusudia .

**66. GIDDY:** Kwa hiyo unasema, mtu anapasa kutumia pesa hizo kwa malengo yaliyokusudiwa?

**67. U. BARRY:** Ndio.Na isitoshe baada ya kuchukua mkopo huo, lipa mara moja unapopata pesa. Lakini ukianza kuahirisha malipo hayo, bila shaka pesa hizo zitapata matumizi mengine na kisha kushindwa kabisa kulipa mkopo huo.

***KW end***

**68. GIDDY:** Sasa una ushauri gani kwa watu waliozoea kuchukua mikopo?

**69. U. BARRY:** Unapoona mkopo unaochukua huishia kwenye pombe, au kucheza kamari, tafadhali tafuta ushauri haraka iwezekanavyo! Unaweza kwenda kwa daktari kwa ushauri au mtu unayekufahamu vyema, ambaye anaweza kukushauri! …Kupitia ushauri unaweza kuepukana na mzigo wa madeni. Inasaidia sana!

**70. GIDDY:** Hebu niambie, siku hizi una maduka mangapi ya kuuza mboga?

**71. U. BARRY:** Duka moja tu...! Lakini nimesambaza huduma hizi, sasa nauza bidhaa zangu kwenye mahoteli na migahawani jijini!

**72. GIDDY:** Na umeweza kufanya hivyo bila ya kuchukua mkopo?

**73. U. BARRY:** Ndio. Unajua mikopo ni gharama na kisha hatari sana! Lakini ukiwa na maono, mikopo inasaidia sana kuimarisha bishara.

**74. SFX: FOOTSTEPS APPROACH**

**75. JD:** **(Drunk)** Mjomba Barry! Mjomba Barry mwenyewe!

**76. BARRY:** Umelewe tena asubuhi hii kijana?

**77. JD:** Mimi sijalewa mjomba...!. Tafadhali nikopeshe dola 5 angalau nipate pombe. Nitakurejeshea kesho!

**78. BARRY:** Nimekwambia uwe unakunywa maji ya matunda, yaani juisi ni nzuri sana kwako kuliko pombe!

**79. JD:** Kama hutaki kunikopesha ni sawa tu! Wacha niende badala ya kunijaza tumbo na maji ya watoto. Eti ni maji ya matunda! Yuk!

**80. SFX:** **FOOTSTEPS LEAVE**

**81. GIDDY:** Subiri kidogo....! si yule ni JD?

**82. BARRY:** Kwani umemsahau? Ni yeye!

**83. GIDDY:** **(Urgently)** Lazima nizungumze naye. **(Gets up, shouts)** JD! JD! Subiri!

**84. SFX:** **GIDDY LEAVING THE GROCERY**

**85. SFX:** **RUNNING FOOTSTEPS, VILLAGE AMB**

**86. JD:** Wacha, wewe kijana wa mjini!. Mimi sikujui, na hujawahi kutukopa .

**87. GIDDY:** (laughs) Mimi ni kijana wa mtaani! Mimi ni yule rafiki yako wa zamani, Giddy!

**88. JD:** **(bleches)** Kidy?

89. **GIDDY:** Gideon Leboo? Tulikuwa shuleni pamoja? Tumbo tumbo? Unanikumbuka sasa?

90. **JD:** **(happy)** Oooh tumbo tumbo! Na unazidi kuwa mkubwa tu kila siku! Nafurahi sana kukuona! Unataka kuninunulia pombe katika klabu hii ya Kwanza!

91. **GIDDY:** **(hesitates)**

92. **JD:** Ni sawa rafiki yangu twende!

## <u>SCENE FOUR: AT KWANZA PUB</u>

93. **SFX: BAR AMBIENCE.**

94. **JD:** **(Roars)** Brr! Nimerudi!

95. **DRUNK 1:** Oh! Umerudi, bingwa wa Karate!

96. **DRUNKS:** **LAUGH.**

97. **MAMA PIMA:** **(Shouts from behind the counter)** Nimekwambia ninii JD. Nimekwambia sitaki kukuona hapa bila kunilipa pesa zangu! Toka nje haraka!

98. **JD:** Una shida gani wewe mwanamke?

***KW begin***

99. **MAMA PIMA: (Stern)** Nakutahadharisha! Nikitoka hapa kwenye kaunta, usinilaumu!

100. **GIDDY:** Sawa mama nitakulipa. Ni shilingi ngapi?

101. **MAMA PIMA: (Unfriendly)** Dola 15!

102. **JD:** **(Shocked)** Eti pesa ngapi? Unataka kutuibia..?, Wewe mama ni tapeli. Dola 12 ama 15! .....

***KW end***

103. **GIDDY:** Ni sawa, JD! **(to Mama Pima)** Shika pesa hizi hapa dola, 15 mama!

104. **JD:** Sawa! Hapa niko na benki yangu! Ulifikiri siwezi kukulipa! Nipe pombe! Pesa zipo!

105. **GIDDY:** Mimi nitakunywa soda tu!

106. **JD:** **(Disgusted)** Pah! Soda! Kwani wewe ni mtoto!

107. **GIDDY:** JD, keti. Nataka kuongea na wewe.

108. **JD:** Kuhusu nini, tajiri wangu?

109. **GIDDY:** Nataka tuzungumze jinsi gani tunaweza kusaidiana.

110. **JD:** Kunisaidia ? **(Laughs sarcastically)** Unataka kunisaidia mimi? **(Bursts out crying)** Huwezi kunisaidia mimi, hebu nitazame vizuri! Maisha yangu yameharibika. Naonekana

Mzee na maskini zaidi, kisha unazungumza mambo ya kutaka kunisaidia … ah...

**111. GIDDY:** Shh! JD! Punguza hasira! Kesho asubuhi, nataka ufike katika duka la mjomba Barry. Bado hatujachelewa, unaweza kubadilika! Bado unaweza kurudia maisha yako ya kawaida!

**112. SFX: GIDDY LEAVES PUB**

**<u>OUTRO:</u>**

**113. SFX: VILLAGE AMB**

**113. NARRATOR:**

JD, JD, Haiwezekani kwamba matumaini yake ya kuwa na maisha mazuri yamedidimia! Namfahamu kuwa kijana mwerevu sana. Na hakika kesho atafika dukani kwa mjomba Barry. Nitajaribu kumsaidia kama rafiki! Na hilo ndilo suala muhimu nalotaka kulishughulikia kwa sasa wakati tunapofika kilele cha mchezo huu wa redio ulioandikwa na James Muhando. Ni matumaini yangu umeufurahia sana mchezo huu! Na tafadhali nakuomba ukumbuke mambo mawili: Kwanza mikopo yote ni hatari, ni jambo la kubahatisha! Na pili ni wosia wa mamangu: **(mimics the voice of his mother)** asilimia *99% ya matatizo yetu hutokana na tabia ya kuiga maisha*

*ya wengine.'* **(Laughs)** Na kwa kuwa sasa ni mtu mzima, nafahamu kwamba yote aliyokuwa akiyasema mama ni ya kweli.

Hadi hapo tunafika mwisho wa mchezo huu. **Starehe za kuazima-Tatizo la kulipa Mkopo**. Ukipenda kukisikiliza tena kipindi hiki basi tembelea mtandao wetu wa dw.de/lbe. Hadi wakati mwengine, tutakapokutana kwa mchezo mwengine wa Noa Bongo Jenga Maisha Yako. Kwaheri kwa sasa.